# Nia Dhidi Ya Kristo – Je Unamheshimu?

# (Attitude Towards Christ – Do you Honor Him?)

**Na**

**Ellis P. Forsman**

# Nia Dhidi Ya Kristo – Je Unamheshimu?

**Na**

**Ellis P. Forsman**

**Octoba 6, 2011**

# Nia Dhidi Kristo – Je Unamheshimu?

## Yohan 5:23

Hakika nia njema hua ni muhimu. Ni muhimu katika kusanyiko la mahali Fulani. Karama zote katika ulimwengu huu haziwezi kuunda nia mbaya ambazo tunaweza kuwa nayo.

Mit. 23:7, "*Maana aonavyo nafsini mwake, ndivyo alivyo. Akuambia haya kla kunywa; lakini moyo wake hauwi pamoja nawe.*"

Nia hutafsiriwa kama: Ni hali ya akili au hisia, kutokuwa sawa.

Kwa maneno mengine, ni hali ya mtu kutambua kitu.

Moja ya vitu katika maisha haya ni nia njema ya kumtii Yesu Kristo.

Yoh. 5:23, "*Ili watu wote wamheshimu Mwana kama vile wanavyomheshimu Baba. Asiyemheshima Mwana hamheshimu Baba aliyempeleka.*"

Vitu vitatu vinafundishwa katika kifungu hiki kifupi.

Vitu viwili kimsingi vinaelezewa.

- "*Ili watu wote wamheshimu Mwana kama vile wanavyomheshimu Baba.*" Yesu alisema yuko sawa na Mungu. Yohana 10:30, "*Mimi na Baba tu umoja.*"
- "*Asiyemheshimu Mwana hamheshimu Baba aliyempeleka.*" Njia pekee ya kumfikia Baba ni kupitia Mwana. Yoh. 14:6, "*Yesu akawaambia mimi ndimi njia, na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba ila kwa njia ya mimi.*" Na yeye amkatae Mwana pia humkataa Baba. Yoh. 12:48, "*Yeye anikataaye mimi asiyeyakubali maneno yangu, anaye amhukumuye, neno hilo nililolinena ndilo litakalomhukumu siku ya mwisho.*"

Kitu kimoja kinahitimishwa:

Kumheshimu Mwana ni kumheshimu Baba.

Hebu na tujifunze jinsi ya kumheshimu Mwana ili kwamba tuweze kumheshimu Baba pia.

Tunamheshimuje Kristo? Hebu tuangalie njia tofauti za kumheshimu Kristo ambazo zimeonyeshwa kwenye maandiko.

# Tunamheshimu Kristo Kwa Kuungama Vyema

1 Tim. 6:12-13, "*Piga vita vile vizuri vya imani; shika uzima ule wa milele ulioitiwa, ukaungama maungamo mazuri mbele ya mashahidi wengi. Nakuagiza mbele ya Mungu anayevihifadhi hai vitu vyote, na mbele ya Kristo Yesu aliyeyaungama maungamo mazuri yale mbele ya Pontio Pilato,*" ni maungamo mazuri yapi ambayo Yesu aliyafanya? Maungamo mazuri yalikuwa kwamba Yesu alikiri kwamba alikuwa Mwana wa Mungu.

Mk. 14:61-62, "*Lakini akanyamaza wala hakujibu neno. Kuhani Mkuu akamwuliza tena akamwambia, wewe ndiwe Kristo Mwana wake Mtukufu? Mimi ndiye, nanyi mtamwona Mwana wa Adamu ameketi mkono wa kuume wa nguvu, akija na mawingu ya mbinguni.*"

Pia aliungama kwamba yeye ni Mfalme.

Yoh. 18:36-37, "*Yesu akajibu, Ufalme wangu sio wa ulimwengu huu. Kama ufalme wangu ungekuwa wa ulimwengu huu, watumishi wangu wangenipigania, nisije nikatiwa mikononi mwa Wayahudi, lakini ufalme wangu sio wa hapa. Basi Pilato akamwambia, basi wewe u mfalme basi? Yesu akajibu, wewe wasema kwa kuwa mimi ni mfalme. Mimi nimezaliwa kwa ajili ya haya, na kwa ajili ya haya mimi nilikuja ulimwenguni, ili niishuhudie kweli. Kila aliye na hiyo kweli hunisikia sauti yangu.*"

Kwa ungamo hili alikufa.

Petro alifanya ungamo kwamba Yesu ni Kristo. Mat. 16:16, "*Simoni Petro akajibu akasema, wewe ndiye Kristo Mwana wa Mungu aliye hai.*"

Yohana alikiri vyema na akaandika kitabu chote ili kuiunga mkono. Yoh. 20:30-31, "*basi kuna ishara nyingine nyingi alizozifanya Yesu mbele ya wanafunzi wake zisizoandikwa katika kitabu hiki. Lakini hizi zimeandikwa ili mpate kuamini kwamba Yesu ndiye Kristo, Mwana wa Mungu; na kwa kuamini mwe na uzima kwa jina lake.*"

Towashi wa Kushi aliungama ungamo hili. Mdo. 8:36-37, "*Wakawa wakiendelea njia wakafika mahali penye maji; yule towashi akasema tazama maji haya ni nini kinachonizuia nisibatizwe? Filipo akajibu, ukiamini kwa moyo wako wote*

*inawezekana. Akajibu akasema ninaamini kwamba Yesu Kristo ndiye Mwana wa Mungu.*"

Kushindwa kumkiri Kristo mbele za watu ni kutomtii Kristo. Mat. 10:32-33, "*Basi kila mtu atakayenikiri mbele ya watu name nitamkiri mbele ya Baba yangu aliye mbinguni. Bali mtu ye yote atakayenikana mbele ya watu, nami nitamkana mbele ya Baba yangu aliye mbinguni.*"

Watu wote watafanywa kukiri jina la Yesu siku ya mwisho. Fil. 2:11, "*Na kila ulimi ukiri ya kuwa YESU KRISTO NI BWANA, kwa utukufu wa Mungu Baba.*"

Hivyo tunamheshimu kila wakati ungamo lililo zuri.

# Tunamheshimu Kristo Katika Ubatizo Wa Wakristo.

Umuhimu wa ubatizo unaonekana katika ukweli kwamba Kristo alijitoa kwalo. Mat. 3:14-15, "*Lakini Yohana alitaka kumzuia akisema, mimi nahitaji kubatizwa na wewe nawe waja kwangu? Yesu akajibu akamwambia kubali hivi sasa kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote. Basi akamkubali.*"

Watu leo wanadai kwamba ubatizo ni kazi ya wanadamu, hivyo wanakataa kuifanya. Ubatizo sio kwa ajili ya haki yetu, bali ya Bwana.

Umuhimu wa ubatizo pia inaonekana katika ukweli kwamba Yesu aliwaagiza wanadamu wote kubatizwa.

Mat. 28:19, "*Basi enendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na la Mwana na la Roho Mtakatifu;*"

Kwa nini mtu akatae agizo hilo la moja kwa moja.

Mk. 16:16, "*Aaminiye na kubatizwa ataokoka, asiyeamini atahukumiwa.*"

Ubatizo ni muhimu kwa ajili ya wokovu wa nafsi zetu.

Yoh. 14:21, "*Yeye aliye na amri zangu na kuzishika, yeye ndiye anipendaye; naye anipendaye atapendwa na Baba yangu name nitampenda na kujidhihirisha kwake.*"

Tunapokataa ubatizo tunaonyesha hakika kwamba hatumtaki.

Katika ubatizo wa Wakristo kuna picha nzuri ya kifo, maziko, na kufufuka kwa Kristo.

Rum. 6:3-4, "*Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo*

*alivyofufuka katika mauti kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima.*"

Alafu bado kuna wengine husema ubatizo sio muhimu. Pasipo ubatizo Kristo hakai ndani mwetu.

## Tunamuheshimu Kristo Katika Meza Ya Bwana

Luka 22:19-20, "*Akatwaa mkate akashukuru akaumega, akawapa akisema huu ndio mwili wangu unaotolewa kwa ajili yenu, fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu. Kikombe nacho vivyo hivyo baada ya kula; akisema kikombe hiki ni agano jipya katika damu yangu, inayomwagika kwa ajili yenu.*"

Baada ya kanisa kuundwa siku ya Pentekoste, iliendelea katika, "*kuumega mkate*." Mdo. 2:42, "*Wakawa wakidumu katika fundisho la mitume, na katika ushirika, na katika kumega mkate, na katika kusali.*"

Kanisa la Korintho lilishiriki siku kuu hii nzuri, na Paulo aliwakemea wale waliokuwa wakishiri isivyo stahili (1 Kor. Sura ya 10), alafu katika sura ya 11 aliwaagiza jinsi ambavyo walipaswa kula, sawa na jinsi Bwana alivyoagiza kabla.

1 Kor. 11:23-29, "*Kwa maana mimi nalipokea kwa Bwana niliyowapa nanyi, ya kuwa Bwana Yesu usiku ule aliotolewa alitwaa mkate, naye akiisha kushukuru akaumega, akasema huu ndio mwili wangu ulio kwa ajili yenu fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu. Na vivi hivi baada ya kula akakitwaa kikombe akisema kikombe hiki ni agano jipya katika damu yangu; fanyeni hivi kila mnywapo kwa ukumbusho wangu. Maana kila mwulapo mkate huu na kukinywea kikombe hiki mwaitangaza mauti ya Bwana hata ajapo. Basi kila aulaye mkate huo au kukinywea kikombe hicho cha Bwana isivyostahili, atakuwa amejipatia hatia ya mwili na damu ya Bwana. Lakini mtu ajihoji mwenyewe na hivyo aule mkate na kukinywea kikombe. Maana alaye na kunywa hula na kunywa hukumu ya nafsi yake kwa kutokuupambanua ule mwili.*"

Kutoka katika historia ya dunia ya kanisa la kwanza tunakuta kwamba tendo hili lili eneo karne mbili za kwanza baada ya kifo cha Kristo.

Wakristo wana ahadi na Kristo kukutana pamoja katika siku ya kwanza ya juma ili kuumega mkate kwa ukumbusho wa Bwana. Kuikataa ni kutomheshimu Kristo na kumtenda dhambi Mungu.

Heb. 10: 25-26, "*<u>Wala tusiache kukusanyiaka pamoja</u> kama ilvyo desturi yaw engine; bali tuonyane na kuzidi kufanya hivyo, kwa kadiri mwonavyo siku ile kuwa inakaribia. <u>Maana kama tukifanya</u>*

*dhambi kusudi baada ya kuupokea ujuzi wa ile kweli, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi."*

# Tunamheshimu Kristo Katika Kuvaa Jina "Wakristo" Na Kukataa Kuvaa Majina Mengine

Kanisa ni lake Kristo. Mdo. 20:28, "*Jitunzeni nafsi zenu na lile kundi lote nalo ambalo Roho Mtakatifu amewaweka ninyi kuwa waangalizi ndani yake, mpate kulilisha kanisa lake Mungu alilolinunua kwa damu yake mwenyewe*."

Nawaulizeni, damu na nani iliyonunua kanisa? Je! Ni ya Mungu Baba au Mungu Mwana? Ufu. 1:5-6, "*Tena zitokanazo kwa Kristo Yesu, shahidi aliye mwaminifu, mzaliwa wa kwanza wa waliokufa na mkuu wa wafalme wa dunia. Yeye atupendaye na kutuosha dhambi zetu katika damu yake na kutufanya kuwa ufalme na makuhani kwa Mungu naye ni Baba yake, utukufu unayeye milele na milele. Amina.*"

Kwa vile ni damu ya Yesu ndio iliyonunua kanisa, inapaswa kuitwa kwa jina lake.

Mat. 16:18, "*Nami nakuambia wewe ndiwe Petro na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu; wala milango ya kuzimu haitalishinda.*" Jesu aliweka wazi kwamba kanisa ni lake.

Rum. 16:16, "*Salimianeni kwa busu takatifu, makanisa yote ya Kristo yawasalimu.*"

Kanisa la kwanza lilifahamu kwamba kanisa ni la Kristo. Wanafunzi wake waliitwa kwa jina lake katika karne ya kwanza na ndivyo wanavyo paswa kuitwa leo.

Mdo. 11:26, "*Hata alipokwisha kumwona akamleta Antiokia. Ikawa kwa muda wa mwaka mzima wakakusanyika na kanisa na kuwafundisha watu wengi. Na wanafunzi waliitwa Wakristo kwanza hapo Antiokia.*"

Mdo. 26:28, "*Agripa akamwambia Paulo, kwa maneno machache wadhani kunifanya mimi kuwa Mkristo*."

Agripa alifahamu kwamba wanafunzi wa Kristo walijiita wakristo.

1 Pet. 4:15-16, "*Maana mtu wa kwenu asiteswe kama mwuaji, au mwivi, au mtenda mabaya, , au kama mtu ajishughulishaye na mambo ya watu wengine. Lakini ikiwa kwa sababu ni Mkristo asione haya bali amtukuze Mungu katika jina hilo.*"

Petro aliwachukulia wafuasi wa Kristo kama Wakristo.

Kuvaa jina hili ni kumheshimu Kristo, usipofanya hivyo ni kutomtii.

Ninyi waume, labda mkeo analazimisha kuvaa jina la mwanaume mwingine. Hautajisikia kujeruhiwa na kukosewa?

Kati yenu enyi waume hamtakosewa kama wake zenu wanalazimisha kutumia jina lingine tofauti na lako?

Katika Agano Jipya uhusiano wetu na Kristo unafananishwa na ule wa bibi arusi na mume wake. 2 Kor. 11:2, "*Maana nawaonea wivu, wivu wa Mungu; kwa kuwa naliwaposea mume mmoja, ili nimletee Kristo bikira safi.*"

Hivyo tunapaswa, kwamba (sisi mabibi arusi) kuvaa jina la Kristo, bwana arusi wetu, na tukatae kuvaa majinja mengine? Tunapaswa kuona wivu kama wake zetu wanavaa majina ya watu wengine. Kristo hayuko tofauti.

Hata kama kanisa linavaa jina la Kristo haimaanishi kwamba ni bibi arusi wa Kristo. Efe. 5:25-27, "*Enyi waume wapendeni wake zenu, kama Kristo naye alivyolipenda kanisa akajitoa kwa ajili yake, ili kusudi alisafishe na kulitakasa kwa maji katika neno; apate kujiletea Kanisa tukufu lisilo na hila wala kunyanzi wala lo lote kama hayo, bali liwe takatifu lisolo na mawaa.*" Efe. 5:32, "*Siri hiyo ni kubwa ila mimi nanena habari ya Kristo na Kanisa.*

Sasa kanisa ni bibi arusi wa Kristo na linapaswa kuvaa jina lake, sawa na jinsi wanandoa wamekuwa wakifanya tangu mwanzo. Mwanzo 5:2, "*Mwanamume na mwanamke aliwaumba akawabariki* ***akawaita jina lao Adamu,*** *siku ile walipoumbwa.*"

Makanisa mengi ya kidunia wanajiita wakristo. Wanavaa jina sahihi, lakini maelezo yao hayafanani na maelezo ya bibi arusi wa Kristo.

Kaka yangu Evart ana jina la mwisho kama langu – Forsmana. Mke wake aitwaye Becky pia anatumia jina ilo hilo, hata kama Becky Forsman anatumia jina kama langu, yeye sio mke wangu. Hafanani na bibi arusi wangu. Hivyo, hata kama kanisa linatumia jina sahihi, bado sio bibi arusi wa Kristo kama haiku katika mfumo ambao Biblia inaeleza.

## Tunamheshimu Kristo Kwa Kujitengeneza Wenyewe Kulingana Na Mfumo Wa Agano Jipya

Maandishi makubwa katika Biblia nyingi kweli utuambia kwamba ni "Agano Jipya la Bwana wetu na Mwokozi Yesu Kristo." Hivyo basi, kama tunaitaji kumheshimu, lazima tulieshimu agano

jipya kwa kuangalia mfumo sisi wenyewe katika kila kitu kulingana na utakatifu wa matakwa yake.

Mfumo mzuri huo utapatikana katika maisha na huduma ya Musa. Mungu alipenda kukaa miongoni mwa watu wake, Israeli, na katika hatima hiyo aliwaagiza kutengeneza hema na madhabahu.

Bali kwa vile ilikuwa ni sehemu Mungu alikuwa anakaa, haikutengenezwa na binadamu, hivyo Mungu akamchukua Musa hadi juu ya mlima na akamfunulia mpango wote wa madhabahu.

Kut. 25:9, "*Sawasawa na haya yote nikuonyeshayo mfano wa maskani na mfano wa vyombo vyake vyote, ndivyo mtakavyoifanya.*"

Kama Musa kwa njia yo yote angeacha mfano huu, je Mungu angemfurahia? Hakuna ambacho kingebaki katika fikira na utengenezaji, hata kwa mtu huyu mwema wa Mungu, bali agizo lilichukuliwa hadi katika vyombo vya madhabahu. Kut. 25:40, "*Nawe angalia ya kwamba uvifanye kama mfano wake, ulioonyeshwa mlimani.*"

Ndivyo ilivyo hata na sisi, kama tunavyotafuta kuishi maisha ya Ukristo na kukutana pamoja katika ibada, tunapaswa kufanya mambo yote kulingana na mfano uliofunuliwa katika Agano Jipya.

# Tunamheshimu Kristo Kwa Kutafuta Kumuiga

Waf. 2:5, "*Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu ambayo ilikuwamo pia ndani ya Kristo Yesu.*"

## Yesu hakuja kufanya mapenzi yake mwenyewe, bali mapenzi ya Mungu.

- Yoh. 6:38, "*Kwa kuwa mimi sikushuka kutoka mbinguni ili niyafanye mapenzi yangu, bali mapenzi ya aliyenipeleka.*"
- Luk. 22:42, "*Akisema Ee Baba ikiwa ni mapenzi yako, uniondolee kikombe hiki, walakini si mapenzi yangu, bali yako yatendeke.*"

Tusipokuja kwa Kristo kwa nia kama hiyo, tutapotea, kwa sababu Kristo anawakubali wale waliotayari kukubali aongoze kusudi la uhai wao.

## Hakuja kutumikiwa, bali kutumika.

Mat. 20:26-28, "*Lakini haitakuwa hivyo kwenu, bali mtu ye yote anayetaka kuwa mkubwa kwenu na awe mtumishi wenu; na mtu ye yote anayetaka kuwa wa kwanza kwenu na awe mtumwa wenu; kama vile Mwana wa Adamu asivyokuja kutumikiwa, bali kutumika na kutoa nafsi yake iwe fidia ya wengi.*"

Huu ndio ulikuwa mfumo mkuu wea maisha yake.

Aliacha mbingu ili awaokoe wengine. Luka 19:10, "*Kwa kuwa Mwana wa Adamu alikuja kutafuta na kuokoa kile kilichopotea.*"

Alijitoa nafsi yake kwa ajili ya wengine wakati wa huduma yake. 1 Pet. 2:21, "*Kwa sababu ndio mlioitiwa, maana Kristo naye aliteswa kwa ajili yenu, akawaachia kielelezo mfuate nyayo zake.*"

Alijitoa msalabani kwa ajili yaw engine.

- Isa. 53:4-6, "*Hakika ameyachukua masikitiko yetu, amejitwika hizuni zetu lakini tulimdhania ya kuwa amepigwa, amepigwa na Mungu na kuteswa. Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu; adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake, na kwa kupigwa kwake sisi tumepona. Sisi sote kama kondoo tumepotea; kila mmoja wetu amegeukia njia yake mwenyewe; na BWANA ameweka juu yake maovu yetu sisi sote.*"

- Gal. 1:4, "*Ambaye alijitoa nafsi yake kwa ajili ya dhambi zetu, ili atuokoe na dunia hii mbovu iliopo sasa, kama alivyopenda Mungu Baba yetu.*"

Mfumo huu lazima ututie msukumo wa kumtumikia Mungu, la sivyo hatumheshimu Kristo.

## Kristo alikuwa mtiifu.

Heb. 5:8-9, "*Na ingawa ni Mwana, alijifunza kutii na mates ohayo yaliyompata; naye alipokwisha kukamilishwa akawa sababu ya wokovu wa milele kwa watu wote wanaomtii.*"

## Kristo alikuwa mnyenyekevu.

Yoh. 13:13-16, "*Ninyi mwaniita Mwalimu na Bwana, nanyi mwanena vyema kwa maana ndivyo nilivyo. Basi ikiwa mimi niliye Bwana na Mwalimu, nimewatawadha miguu, imewapasa vivyo kutawadhana miguu ninyi kwa ninyi. Kwa kuwa nimewapa kielelezo ili kama mimi nilivyo watendea, nanyi mte vivyo. Amin, amin, nawaambia ninyi mtumwa si mkuu kuliko bwana wake; wala mtume si mkuu kuliko yeye aliyempeleka.*"

## Kristo alikuwa mtu wa maombi.

Alianza huduma yake kwa maombi. Luk. 3: 21-22, "*Ikawa watu wote walipokwisha kubatizwa na Yesu naye amebatizwa, naye anaomba mbingu zilifunuka; Roho Mtakatifu akashuka juu yake kwa mfano wa kiwiliwili, kama hua sauti ikatoka mbinguni, Wewe ndiwe Mwanangu mpendwa wangu; nimependezwa nawe.*"

Aliendeleza kwa maombi, kwa sababu mara nyingi tunakuta anaomba wakati wa huduma yake. Alihitimisha huduma yake kwa maombi. Luk. 23: 46, "*Yesu akalia kwa sauti kuu, akasema Ee Baba, mikononi mwako naiweka roho yangu.*"

Tunapaswa kumuiga na kuwa na maisha yalijaa sala.

Omba bila kukoma. Tumuhusishe katika maisha yetu milele, shida na maamuzi.

# Hitimisho

Kama wewe sio Mkristo, kwa nini usije kwa Yesu sasa kulingana na mfano tuliouona katika Agano Jipya (Kusikia, Imani, Toba, Kukiri, na Ubatizo)? Alafu unaweza kwenda zako ukifurahi, kama towashi wa Kushi alivyofanya.

Masamaha wa dhambi zako utakuwa hakika na taraja la uzima wa milele utakaa katika msingi ambao hauwezi kutetereka.

Je wewe ni Mkristo? Au unakaribia kuwa mkristo?

Mtu anafanyikaje Mkristo? Zifuatazo ni hatua muhimu zinazofanya hilo liwezekane:

- **Imani.** Waeb.11:6, *"Maana pasipo imani haiwezekani kumpendeza, kwa maana yeye ajye kwa Mungu lazima aamini kwamba yeye ndiye, na kwamba huwapa dhawabu wale wote wamtafutao."* Nilipokuwa shuleni (nikiwa na miaka 17) kijana mmoja jirani yangu miaka sawa na ya kwangu aliniambia kuwa aamini katika Mungu. Kwa vile nilikuwa nimebatizwa, nikachukua muda wa kuongea naye kuhusu maandiko. Akaniambia kwamba anaweza kuona kwamba kuishi maisha ya Ukristo ilikuwa nzuri, lakini hakuwa na uhakika kwamab kuna Mungu. Lakini ilikuwa sehemu yenye usalama, niheri aende kanisani, na akifa na kusimama mbele za Mungu (kama kuna Mungu) katika siku ya hukumu (kama kuna hukumu), labda Mungu atamuruhusu aingie mbinguni (kama kuna mbingu), na siyo motoni (kama kuna moto). Nikamwambia, "haifanyi kazi kwa njia hiyo. Lazima uamini katika yeye kwa moyo wako wote la sivyo huwezi kumpendeza.

- **Toba.** Matend. 2:38, *"Petro akawambia tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu kwa jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."* Matend 11:18, *"...Mungu amewajalia hata mataifa nao toba iletayo uzima."* Kama ulikuwa unalala, ukasikia kelele kwenye chumba nyingine, ukafikiria mwenyewe, "kuna mwizi humu ndani!" Na unachukua simu yako na kuwa pigia polisi, ukiwambia kuwa kuna mwizi nyumbani kwako. Muda mfupi unasikia wanafika na kumshika mwizi. Anapiga kelele, "samahani; samahani!" Anaomba msamaha wa nini? Anaomba msamaha kwa sababu amekamatwa; si kwamba ameiba. Katika toba ya kweli mwizi lazima aombe msaha kwamba hataiba tena na kubadilisha maisha yake. Ni badiliko la nia linalo leteleza badiliko la matendo. Hicho ndicho tunachotakiwa kufanya kabla hatujawa Wakristo.

- **Kukiri.** Waru. 10:9-10, *"Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu."* Tunakiri nini? Kwamba tunaamini kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu.

  Kumbuka kwamba kifungu hicho kwamba imani (kuamini), kutubu, na kukiri ni "**KATIKA**" haki, uzima au wokovu. "Katika" inamaanisha kuelekea kitu Fulani; siyo kwamba tayari amesha pata.

- **Ubatizo.** Ni katika ubatizo ndipo haki, uzima, na wokovu vinapatikana. Yesu, mwenyewe, alibatizwa ili kuitimiza haki yote, "*Lakini Yohana alitaka kumzuia, akisema, mimi nahitaji kubatizwa na wewe, nawe waja kwangu? Yesu akajibu akamwambia kubali hivi sasa. Kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote. Basi akambatiza. Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini na tazama mbingu zikamfunukia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua akija juu yake; na tazama sauti kutoka mbinguni ikisema, Huyu ni mwanangu mpendwa wangu, ninayependezwa naye."* (Math. 3:14-17).

  Yesu alibatizwa kwa sababu Mungu alisema ni jambo zuri kufanya. Unaona ni jinsi gani ilivyompendeza Mungu Yesu alipobatizwa? Yesu pia akasema "imekuwa kwetu **sisi** "*kuitimiza haki yote*" Tunabatizwa kwa sababu inatimiza haki yake yote, siyo kwa sababu ni haki yetu.

Hakika, tusipobatizwa, bado tungali katika dhambi zetu. *"Petro akawambia tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu katika jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."* (Matend. 2:38). Petro, umesema ni nini maana ya ubatizo? "kwa ajili ya ondoleo la dhambi." Kwa nini yeyote anaweza kuacha hatua inayotuondoa dhambi?

Yesu aliamuru kwamba ili kuufikia wokovu lazima tuzikwe. "*Na akawambia enendeni ulimwenguni kote mkahubiri injili kwa kila kiumbe. Aaminiye **na** kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa."* (Marko 16:15-16).

Anania alimwambia Paulo (kabla hajaitwa Paulo) kitu kile kile *"Sasa unakaawilia nini? Simama, na ubatizwe ukaoshwe dhambi zako, ukiliitia jina la Bwana."* (Matend. 22:16).

Ubatizo ni hitaji lililotolewa na Mungu.

Ubatizo unaitwa maziko. *"Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake: kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima."* (Waru 6:4). Utu wetu wa kale lazima ufe. *"Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima. Kwa maana kama mlivyounganika kwa mfano wa kufufuka kwake; mkijua neno hili, ya kuwa utuwetu wa kale ulisulubishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusitumikie dhambi tena."* ( Waru. 6:3-6). Ubatizo ni ramani yake Mungu kwa kupaka damu yake Kristo katika maisha yetu kwa ubatizo. Tuko huru na dhambi zetu za zamani pale tu tunapobatizwa.

Hii haimaanishi "kunyunyiza. Andiko hilo hapo juu linasema ubatizo ni maziko. Hatuziki mwili kaburini kwa kuweka udongo mdogo juu yake; tunazika mwili.

Kama hujawa Mkristo, kwa nini usizingatie leo?